

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO

16 JUNI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO – TAREHE 16 JUNI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023 na Tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

396. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatoa kiasi cha fedha ilizoahidi kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Malula Kibaoni hadi Ngarenanyuki.

397. MHESHIMIWA MWITA KEMBAKI MICHAEL (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza michango kwa Wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha kwanza.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

398. MHESHIMIWA MWANTUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Dunga.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

399. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe ili Wananchi waweze kupata huduma.



WIZARA YA AFYA:

400. MHESHIMIWA SANTI EL ERICK KIRUMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itaboresha kitengo cha Watoto njiti katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
16 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**